JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BIHARAMULO

12/02/2023

TANGAZO LA ZABUNI

KWA AJILI YA KUJENGA MAJENGO YA HOSPITALI YA WILAYA YA BIHARAMULO-ENEO LA KIJIJI CHA KATOKE

Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali ya Hospitali ya Wilaya ya kutolea huduma ya afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kutokana na kupata fedha hizo ujenzi wa majengo yafuatayo unatarajia kuanza mwezi Machi mwaka 2023.

Majengo hayo ni kama ifuatavyo:

- Jengo la wodi ya Wanawake (Female Surgical Ward)
- Jengo la Kuhifadhia maiti (Mortuary)
- Jengo la Wodi ya Watoto (Pediatric Building)
- Jengo la wodi ya Wanaumme (Male Surgical Ward)
- Ukamilishaji wa jengo la kufulia,Utawala,Mionzi, Famasi na Wazazi) na
- Ujenzi wa mfumo wa Maji taka

Kwa kuwa njia ya ujenzi itakayotumika ni ya kutumia Wataalamu wa ndani na kununua vifaa (**force account**); Hivyo basi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilayani Biharamulo chini ya sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kanuni Na.181 anawatangazia ***Wananchi, Makampuni, Taasisi na Vikundi mbalimbali*** kuomba zabuni katika **UJENZI WA MAJENGO YA HOSPITALI YA WILAYA** kama ifuatavyo:-

Fungu Na.	**Maelezo** *[Orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji]*
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.1	Fundi Ujenzi jengo la kuhifadhia maiti
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.2	Fundi Ujenzi jengo la Wodi ya Watoto
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.3	Fundi Ujenzi jengo la Wodi ya Wanawake
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.4	Fundi Ujenzi jengo la Wodi ya Wanamme
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.5	Fundi wa kufunga mfumo wa maji safi na taka jengo la kuhifadhia maiti, wodi ya Watoto,wodi ya wazazi,upasuaji wanawake na wanamme
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.6	Fundi Umeme wa kuweka mfumo wa umeme jengo la kuhifadhia maiti,Wodi ya Watoto,wodi ya wazazi, upasuaji wanawake na wanamme
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.7	Fundi Ujenzi wa mashimo ya Maji taka na safi kwenye majengo
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.8	Fundi wa uwekaji wa Epoxy jengo la Wodi ya Wazazi
LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.9	Fundi ujenzi ukamilishaji wa jengo la wodi ya Wazazi

LGA/032/2022-2023/HQ/W/01/LOT.10	Fundi ujenzi ukamilishaji wa jengo la famasi,mionzi,Utawala na kufulia.

SIFA ZA MWOMBAJI

a) Awe Mtanzania mwenye Kitambulisho cha Mpiga Kura au cha Taifa au Leseni ya Udereva au Hati ya kusafiria na apatikane kirahisi wakati wa kutekeleza kazi.

b) Awe na utambulisho kutoka ofisi ya kijiji/Mtaa au kata anayoishi

c) Awe amesajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

d) Awe na uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali

e) Awe na uwezo au uzoefu wa kusoma na kutafsiri sahihi michoro, vipimo na uwiano wa vifaa vya ujenzi.

f) Aambatanishe Cheti kinachohusiana na kazi anayoomba cha VETA, Diploma, FTC,Degree na zaidi.

g) Ajaze bei/gharama anazoomba kwa ajili ya kazi atakayoifanya (Schedule of Labour)

h) Aambatanishe Mikataba ya ufundi na Cheti cha kumaliza kazi ambayo amewahi jenga majengo ya Serikali na anuani zake.

i) Awasilishe mpango kazi wake akionyesha mtiririko wa shughuli pamoja na muda atakaoutumia kukamilisha kazi ya ujenzi kwa muda usiozidi miezi mitatu.

j) Awe na mtaji wa kutosha kwa maana ya rasilimali watu na vitendea kazi muhimu kama vile futi, pima maji n.k

k) Awe na uwezo wa kuwalipa mafundi na vibarua watakaomsaidia kazi kabla ya malipo yake kufanyika, malipo yatafanyika mara baada ya Meneja mradi kuridhika na ubora wa kazi husika.

Aina ya kazi zitakazofanyika:

i. Kujenga Msingi wa Jengo (Sub-structure)
ii. Kunyanyua jengo (Super-structure)
iii. Kuezeka (Roofing structure and covering)
iv. Kusimika fremu na kufunga milango
v. Umaliziaji (Finishing)
vi. Kupaka rangi na Mapango (Painting and Decoration)
vii. Kuweka umeme (Electrical installation)
viii. Kuweka mfumo wa maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)
ix. Ujenzi wa mashimo ya maji safi na taka kwenye majengo.

NB: Fundi Mmoja Hatapewa kazi zaidi ya Moja hata kama amekidhi vigezo vilivyoorodheshwa hapo juu.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE WENYE SIFA NI KAMA IFUATAVYO

1. Waombaji wanatakiwa kuja kuchukua nyaraka ya zabuni wanayotaka kuiomba katika **Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kilichopo katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo** mara baada ya kulipia ada ya zabuni ya kiasi cha Tsh 30,000.00 ambayo **haitarejeshwa**.(*Mwombaji afike Ofisi ya Mwekahazina Wilaya ili apewe control number ya kulipia hayo maombi*)
2. Mwombaji ahakikishe fomu zote za maombi ya zabuni zimejazwa kwa uhakika bila kukosewa.
3. Maombi yote yaambatanishwe na barua ya maombi ya zabuni yenye taarifa ya njia za mawasiliano kama vile namba za simu, Majina mawili ya Wadhamini, barua pepe au anwani za makazi pamoja na risiti ya malipo ya maombi kwa kila ombi la zabuni.
4. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyo kamilika, maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa na zoezi la uchambuzi wa kumpata mzabuni.
5. Maombi yanatakiwa kufungwa kwenye bahasha na kuonesha aina ya zabuni inayoombwa bila kuwa na viashiria vyovyote inakotoka na yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO
S.L.P. 70,
BIHARAMULO.

Muda wa mwisho wa kupokea Maombi ni **saa nne (4) kamili asubuhi** (4:00) (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **20/02/2022** siku ya **jumatatu na zabuni zitafunguliwa saa 4:30** katika **Ukumbi wa Mikutano** wa Halmashauri ya **Wilaya ya Biharamulo.** Waombaji au wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria kwenye ufunguzi. Baada ya ufunguzi taratibu zingine za manunuzi zitafuata.

Imetolewa na;

.....

INNOCENT M.MUKANDALA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BIHARAMULO